MARA
S. L. P 377
Simu 028 2620240
Nukushi 028 2620012

MBEYA
S. L. P 1419
Simu 025 25603566
Nukushi 025 2502958

MOROGORO
S. L. P 845
Simu 023 2614302
Nukushi 023 2614478

MTWARA
S. L. P 213
Simu 023 2334013
Nukushi 023 2333726

MWANZA
S. L. P 2599
Simu 028 2500600/2
Nukushi 028 2500602

NJOMBE
S.L.P 629
Simu 026 2782777
Nukushi 026 2782777

PWANI
S. L. P 30261
Simu 023 2402658/2402284
Nukushi 023 2402657

RUKWA
S. L. P 273
Simu 025 2802426/2802926
Nukushi 025 2800312

RUVUMA
S. L. P 926
Simu 025 2600613
Nukushi 025 2600663

SHINYANGA
S. L. P 37
Simu 028 2762630
Nukushi 028 2763358

SIMIYU
S. L. P 306
Simu 028 2700371
Nukushi 028 2700532

SINGIDA
S. L. P 484
Simu 026 2502305/2502550
Nukushi 026 2502550

TABORA
S. L. P 1020
Simu 026 2604030/2604311
Nukushi 026 2604039

TANGA
S. L. P 1953
Simu 027 2645186
Nukushi 027 2647885

TEMEKE
S. L. P 42325
Simu 022 2863092

MKURUGENZI MKUU

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa
S.L.P 4865

Dar es Salaam.Simu: 022-2150043-6
Nukushi: 022-2150047
Baruapepe: dgeneral@pccb.go.tz
Wavuti: www.pccb.go.tz

SIMU YA BURE : 113

JUKUMU LA KILA MWANANCHI KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mwananchi mwenye uzalendo wa kweli na anayeipenda nchi yake huwa mstari wa mbele katika kupambana na rushwa, bila woga wowote. Uzalendo ni kuitetea nchi hadi kujitoa kufa kwa ajili yake huku ukitetea haki, utamaduni, mali za nchi pamoja na mambo yote yanayowafanya kuwa wamoja katika taifa. Bila kumnyooshea kidole mtu mwingine mwananchi unatakiwa kuchukua hatua pale unapoona mtu anavunja sheria, kwa kupokea rushwa au kwenda kinyume na maadili ya kazi. Katiba ya nchi Ibara ya 26 (2) "Kila mtu ana haki, kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria, kuchukua hatua za kisheria kuhakikisha hifadhi ya katiba na sheria za nchi".

JINSI YA KILA MWANANCHI KUSHIRIKI KUPAMBANA NA RUSHWA

Kila mwananchi ana wajibu wa kushiriki katika kuzuia na kupambana na rushwa kwa kufanya yafuatayo;

KUTOA TAARIFA

Kila mwananchi ana jukumu la kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa TAKUKURU au kwa vyombo vingine vya sheria au dola.

Ibara ya 27 (2) inasema watu wote watatakiwa na sheria kutunza vizuri mali ya mamlaka ya nchi na ya pamoja, kupiga vita aina zote za uharibifu, na kuendesha uchumi wa taifa kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadae ya taifa lao.

Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na 11 ya mwaka 2007 kifungu cha 39 kinatamka "kila mtu ambaye anafahamu au anafahamu kusudio la kutendwa kwa kosa la rushwa kutoa taarifa kwa afisa wa TAKUKURU". Taarifa zinaweza kutolewa kwa njia ya simu, barua, barua pepe au kufikisha taarifa hizo katika ofisi ya TAKUKURU Makao Makuu au ofisi zilizopo mkoani na wilayani kote nchini.

KUTOA USHAHIDI

Kutoa tu taarifa bila kuwa tayari kutoa ushahidi hakutasaidia kuwachukulia hatua za kisheria wala rushwa. Hivyo wewe mwananchi una jukumu la kuwa tayari kutoa ushahidi wa vitendo vya rushwa ulivyoshuhudia katika Mahakama au popote pale unapohitajika kufanya hivyo. Athari za kukataa kutoa ushahidi au taarifa sahihi ni kesi kushindwa mahakamani au kukosa ushahidi wa kufungua kesi.

KUTOA ELIMU

Mwananchi yeyote una jukumu la kumuelimisha mwananchi mwenzako kuhusiana na suala la rushwa na athari zake kwake yeye na jamii kwa ujumla. Kwa kufanya hivyo utakuwa umesaidia mwananchi huyo kuepuka kujihusisha na vitendo vya rushwa. Vilevile kwa kushiriki kutoa elimu utakuwa umeunga mkono juhudi za serikali za kupambana na rushwa nchini na kuisaidia kufikia lengo la kuwa na Tanzania isiyo na rushwa.

KUACHA RUSHWA

Mwananchi unatakiwa kuichukia rushwa na kuepuka kushiriki vitendo vya rushwa. Rushwa ni kikwazo kikubwa kwa demokrasia, utawala bora, haki za binadamu na ni tishio kwa amani, utulivu na usalama katika jamii. Wewe ndiye unayeathirika zaidi katika kila tendo la rushwa unaloshiriki, hivyo AMKA, ACHA RUSHWA!

KUTII SHERIA

Mwananchi, ni lazima uishi kwa kutii sheria, kanuni na taratibu za nchi pamoja na kuunga mkono juhudi za serikali za kuzuia na kupambana na rushwa. Mwananchi unatakiwa kubadili mawazo na mtazamo kwamba mapambano dhidi ya rushwa ni ya TAKUKURU au vyombo fulani peke yake. Ushirikiano wako na TAKUKURU pamoja na wadau wengine ndio njia pekee itakayosaidia kuleta mafanikio katika kutokomeza rushwa.

Amka Mwananchi, Bila Rushwa - Maendeleo ni hakika kwa asilimia 100

MKUU WA TAKUKURU MKOA

ARUSHA
S. L. P 1055
Simu 027 2503538, 027 2507928
Nukushi 027 2505973

DODOMA
S. L. P 1175
Simu 026 2322003/2322695
Nukushi 026 2320003

GEITA
S. L. P 38
Simu 028 2520040
Nukushi 028 2520040

ILALA
S. L. P 6420
Simu 022 2861088
Nukushi 022 2150047

IRINGA
S. L. P 1575
Simu 026 2700156
Nukushi 026 2703014

KAGERA
S. L. P. 1138
Simu 028 2220848/2220491
Nukushi 028 2220534

KATAVI
S. L. P. 275
Simu 025 2820613,
Nukushi 025 2820613

KIGOMA
S. L. P 880
Simu 028 2802889
Nukushi 028 2804928

KILIMANJARO
S. L. P 1951
Simu 027 2750885
Nukushi 027 2750889

KINONDONI
S. L. P 90397
Simu 022 2170852

LINDI
S. L. P 1004
Simu 023 2202456/ 2202799
Nukushi 023 22022215

MANYARA
S. L. P 386
Simu 027 530255/2530256/2530570
Nukushi 027 2530448